

Je, nifanye nini ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Hakuna chanjo dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Lakini kuna mienendo ya tabia ambayo i itaweza kukusaidia kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na UKIMWI. Kutokufanya ngono kabisa ni njia mojawapo ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na UKIMWI. Kuwa mwaminifu na kuwa na mpenzi i ambaye hajaambukizwa ni njia nyingine ya kujikinga. Lakini hii i ii inahitaji wote muwe katika afya nzuri (bila maambukizi) wakati mnaanza uhusiano wa kujamii ana kwa mara ya kwanza. Pia i inashauriwa hima kutafuta matibabu ya magonjwa ya ngono mara pale yatakapojitokeza. Vidonda vinavyosababishwa na magonjwa ya ngono vinasababisha mwingiliano wa maji maji ya ukeni, maji maji ya uumeni na damu wakati wa kujamii ana na kuwezesha Virusi vya UKIMWI kupita kwa urahisi. Kufuata kanuni za ngono salama ni njia nyingine ya kujikinga ili usiambukizwe na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Ngono salama kwa upande mwingine ni kitendo cha kukaribiana ambacho hakitahusisha uume kuingia ukeni au njia ya haja kubwa. Pia utumiaji wa kondomu kila wakati ngono i itahusisha kuingizwa kwa umme, ukeni au njia ya haja kubwa ni njia nyingine ya kujikinga

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25932>